# MKATABA WA UPANGISHAJI NYUMBA ILIYOPO KITALU NO. 3 CENTRAL SONGEA MJINI.

Mkataba huu umefikiwa leo hii tarehe...10... Mwezi wa ...11......... 20.23

BAINA YA

**ANGELUS JOACHIM NGONYANI** wa Sanduku la Posta 78388 Songea (na ambaye atajulikana kama mwenye nyumba kwa upande wa kwanza)

NA

**JACKAENGO 2015 LIMITED** wa 507 Songea (ambaye atajulikana kama mpangaji kwa upande wa pili)

**KWAMBA** mwenye nyumba anamiliki nyumba iliyopo Katika Kitalu Na. 3 iliyopo Central Songea Mjini na ana nia ya kupangisha nyumba hiyo kwa mpagaji kadri ya masharti ya mkataba huu.

**NA KWAMBA** mpangaji ameridhika na yupo tayari kupanga hapo kadri ya masharti ya mkataba huu.

**HIVYO BASI** pande mbili wanafikia makubaliano ya kupangisha chumba kwa masharti yafuatayo:-

1) Kwamba Mkataba huu ni wa kipindi cha Miaka Mitatu (3) na utaanza mnamo tarehe 10 Novemba, 2023 na utaisha mnamo tatrehe 09 November, 2026.

2) Mwenye nyumba atapangisha na mpangaji atapanga cnyumba tajwa kwa gharama ya Shillingi Laki Sba Kwa Mwezi (700,000/) yaani jumla ni Shilingi Milioni Ishirini na Tano na Laki Mbili Tu (TSHS. 25,200,000/=).

3) Mpangaji amelipa kiasi cha shilingi TSHS. 25,200,000/= na hakuna kiasi kingine kinachosalia.

4) Mpangaji atahakikisha wakati wote nyumba husika ipo katika hali nzuri kwa kuzingatia vyema usafi wa nyumba pamoja na mazingira yake kwa ujumla na kurekebisha sehemu zozote zinazohitaji marekebisho.

5) Mpangaji ataitumia nyumba husika kwa makazi yake kipindi chote cha mkataba na hatotakiwa kumpangisha mtu mwingine yeyote wakati mkataba huu isipokuwa tu kwa idhini ya mwenyenyumba.

6) Mpangaji atatunza usafi wa mazingira yeye binafsi kwa gharama zake bila ya kumhusisha mwenye nyumba.

7) Mpangaji atamruhusu mwenye nyumba kuingia kwenye chumba na kufanya ukaguzi kwenye nyumba kwa kutoa taarifa mapema juu ya kusudio lake la kutaka kufanya ukaguzi.

8) Mpangaji atagharamikia matumizi ya umeme, maji safi na maji taka katika nyumba husika.

9) Mpangaji hatotakiwa kuitumia nyumba husika kwa namna yoyote ile isiyofaa kimaadili pamoja na kisheria na kujiepusha kusababisha bughudha ya namna yoyote ile.

10)Pande zote mbili zinakubaliana kwamba watakuwa na uhuru wa kusitisha mkataba huu kwa wakati wowote kabla ya kipindi cha mkataba kuisha kwa kutoa taarifa ya miezi miwili juu ya kusudio hilo.

11)Kwamba endapo Mpangaji atataka kuendelea na pango basi atatakiwa kutoa Notisi ya Walau Miezi Miwili (Siku Sitini) juu ya kusudio lake la kuendea na pango. Malipo yoyote ya pango ni sharti yafanywe kupitia Akaunti ya FAMCOM yenye Namba 173218000580 iliyopo Tanzania Commercial Bank (TCB) Tawi la Executive.

12)Iwapo kutatokea kutoelewana baina ya mpangaji na mwenye nyumba kuhusiana na mkataba huu, tofauti zao watazimaliza kwa kutumia njia ya na ikishindikana hapo suala zima lipelekwe vyombo vya sheria.

**MKATABA HUU** umeshuhudiwa na pande mbili wanaohusika kwa kuweka saini na tarehe zao hivi ifuatavyo:-

**IMETIWA SAINI** na **ANGELUS J. NGONYANI** ____________

**MPANGISHAJI**

Tarehe 10/11/2023

**IMETIWA SAINI** na **JACQUELINE KANDIDUS NGONYANI** (Mkurugenzi)
Kny **JACKAENGO 2015 LIMITED** (MPANGAJI)

Saini: ____________

Tarehe: 10/11/2023

JACKAENGO 2015 LIMITED
S. L. P 941
DODOMA
TANZANIA

**KWA USHUHUDA, MKATABA HUU UMESAINIWA NAMI.**

Jina: MPWAGA BERNARD

Saini: ____________

Anuani: 45298 DISALAAM

Tarehe: 10/11/2023

MPWAGA BERNARD
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
P. O. Box 45298, DAR ES SALAAM